

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII**  
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**



**MAELEKEZO KWA WASAFIRI**

**TOLEO LA II, TAREHE: 04 APRILI, 2020**

Tarehe 23.03.2020, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa ushauri wa kitaalam kwa wasafiri kuhusu hatua za kuchukua ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wa COVID-19. Kufuatia maazimio ya kikao cha pamoja cha Mawaziri wa Afya na Mawaziri wenye dhamana masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki cha tarehe 25.03.2020, Serikali ya Tanzania imeboresha ushauri wa Toleo la kwanza ili kujumuisha usafirishaji wa bidhaa na huduma.

Hivyo, maelekezo yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa;

- Watanzania na wageni wanaoishi nchini wanashauriwa kutosafiri kwenda nchi zilizoathirika kama hakuna ulazima huo.
- Wasafiri wote watakaoingia nchini watawekwa kwenye karantini kwa gharama zao kwa muda wa siku 14 katika maeneo yatakayoainishwa na Serikali.
- Utaratibu wa kusafirisha huduma na Mizigo kwenye vyombo vyatua;
- Utaratibu kwenye vyombo vyatua usafiri vilivyobeba mizigo na vyenye kutoa huduma utakuwa kama ifuatavyo;
  - i. Vinatakiwa kuwa na wahudumu wasiozidi watatu (03) waingiapo nchini
  - ii. Vitatakaswa (decontamination) mpakani endapo italazimika.
  - iii. Madereva wa vyombo hivyo watatakiwa kubainisha mwisho wa safari zao (final destinations), na kusimama katika maeneo maalum yaliyotengwa wawapo njiani.

- iv. Wahudumu wa vyombo hivyo, endapo watashukiwa kuwa na COVID-19, watawekwa kwenye eneo tengefu (*Isolation*) katika maeneo yaliyotengwa na Serikali.
  - v. Endapo mhudumu/wahudumu wa vyombo hivyo watawekwa kwenye *Isolation* wakati wakiwa wanaendelea na safari (on-transit), wamiliki watatakiwa kuweka utaratibu wa kupata wahudumu wengine ili mizigo yao iweze kufika katika maeneo husika.
  - vi. Wahudumu wa ndege au meli za mizigo watawekwa kwenye karantini kwenye maeneo yaliyobainishwa na Serikali kwa kipindi chote watakachokuwa nchini.
  - vii. Mashirika ya ndege (Airlines) yanatakiwa kuhakikisha kwamba wana seti mbili za wahudumu (crew) ili kubadilishana baada ya kuingia nchini na kuondoa ulazima wa kuwekwa Karantini.
- Abiria wote watatakiwa kujaza fomu za ufuutiliaji wa masuala ya afya (Traveler Surveillance Form) ndani ya ndege na kuziwasilisha kwenye dawati la Timu ya Afya kwenye mipaka (Port Health authorities) mara tu waingiapo nchini.
  - Wasafiri wote watakaoingia nchini watafanyiwa ukaguzi wa kina ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa vipimo vya COVID-19 pale itakapoelekezwa kufanya hivyo.
  - Baada ya karantini ya siku 14, mhusika ataruhusiwa kutoka kwenye karantini baada ya kuacha maelezo binafsi kwa ajili ya ufuutiliaji wa ziada endapo kutakuwa na uhitaji huo.
  - Endapo msafiri atapata dharura yoyote ya afya, atatakiwa kupiga simu ya bure ya dharura (**Health Emergency Number 199**).

**NB:** Ushauri huu kwa wasafiri utaendelea kuboreshwa mara kwa mara kutokana na mabadilliko ya hali ya ugonjwa hapa nchini.



Ummy A. Mwalimu (Mb),

**Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**